MPANGO SHIRIKISHI WA KUTATHMINI UMASKINI
2002/3

MADA JUU YA HALI INAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKARISHWA[1]

I. **Dhana ya Kuwa katika hatari ya kushuka kimaisha**
II. **Hali au mambo yanayosababisha jamii kufukarishwa**
III. **Mbinu za (mtu binafsi, kaya au jamii) za kujilinda au kujikinga dhidi ya ufukarishwaji**

I: DHANA YA KUWA KATIKA HALI INAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKARISHWA

1. **Watu au jamii huelewa mahusiano kati ya umaskini na kuwa katika hali ambayo inaweza kusababisha kufukarishwa? Kama ndio, ni kwa jinsi gani? Kama sio, kwa nini?**

2. **Ni makundi gani ya watu katika jamii ambayo hufikiriwa kuwa katika hali ambayo inaweza kuwafukarisha kuzidi wengine?**

- Ni makundi gani ya aina hiyo ambayo yanatambuliwa kuwa katika hatari zaidi katika jamii yetu
- Ni mambo gani ambayo jamii inayaona ni muhimu katika kutofautisha kundi moja na jingine kuwa katika hatari hiyo

II: VYANZO NA MATOKEO YA KUKUMBWA NA HALI AU MAMBO YANAYOSABABISHA MTU AU JAMII KUFUKARISHWA

3. **Mazingira na uwezekano wa kufukarishwa**

3.1 Mitazamo ya jamii

- Ni hali gani ya mazingira (kwa mfano: hali ya maliasili; hali ya hewa) ambayo watu huona au hufikiria kwamba vinaweza kusababishia mtu au jamii kufukarishwa.
- Ni kwa njia gani kufukarishwa kunaweza kujitokeza kutokana na hali hii?
- Watu wanaonaje mwelekeo wa hali ya mazingira? – je mazingira yanabadilika? Kwa jinsi gani? Je, serikali nayo inalichukuliaje suala hili?
- Watu wanafikiri ni kwa jinsi gani wao wenyewe pamoja na watunga sera (katika ngazi mbalimbali) wanaweza kupunguza uzito na madhara ya hali ya uharibifu wa mazingira?

[1] PPA (2002/3) Research Agenda on vulnerability

3.2 Uharibifu wa mazingira (mfano:- udongo, malisho, misitu na uvuvi)

- Ni kwa jinsi gani uharibifu wa mazingira unaathiri hali nzuri ya maisha ya makundi mbalimbali (mfano: akina mama na wakulima wadogowadogo) au kuchangia kuwaweka katika hali inayoweza kuwasababishia ufukara?

3.3 Majanga ya asili (mfano: ukame na mafuriko)

- Ni kwa jinsi gani majanga ya asili huathiri maendeleo ya kimaisha ya makundi mbalimbali ya jamii
- Kuna baadhi ya makundi katika jamii ambayo yako katika hatari zaidi ya kufukarishwa kutokana majanga ya asili kuliko makundi mengine?
- Ni jinsi gani ambavyo watu (mtu binafsi, familia, jamii) hujaribu kukabiliana na majanga ya asili
- Ni kwa jinsi gani Serikali inaweza kusaidia mwitikio wa watu katika kupambana na majanga ya asili?
- Hali ya kufukarishwa inandeana na misimu?

4. Njia za Kujikimu kimaisha na hali inayosababisha kufukarishwa

- Ajira ya watoto (wale walio katika umri wa kwenda shule) inasaidiaje familia au kaya kupunguza makali ya umaskini? Watoto wenyewe wanalionaje suala hili? Wanaona hali hii inaweza kuwasababishia ufukara katika maisha yao ya baadae?
- Hatari ya kufukarishwa inayowakabili vijana wasio na ajira maalum (walio mijini na vijijini) ni tofauti na hali inayowakabili watu wengine katika jamii?
- Uwezo wa sehemu fulani ya jamii (mfano: wanawake, wasiojiweza) kushiriki katika njia kadhaa za kujikimu kimaisha unawaweka katika mwanya mkubwa wa kufukarishwa ukilinganisha na watu wengine (mfano wanaume)?
- Ni hatari za aina gani zinazowezesha mtu kufukarishwa zinazowakumba watu mbalimbali au makundi mbalimbali ya jamii?
- Kuna uhusiano gani kati ya milki ya ardhi/kutomiliki ardhi na uwezekano wa kufukarishwa?

4.1 Njia za kujikimu zilizo "hatari" au "zilizo kinyume cha sheria"

- Ni kwa nini watu hujihusisha na njia za kujikimu zilizo "hatari" au "zilizo kinyume cha sheria" (mfano: umalaya, ujangili nk) Kuna uhusiano wowote kati ya mbinu hizi na hali ya ufukarishwaji?
- Ni kwa jinsi gani ajira mbaya sana za watoto husababisha wakumbwe na hali inayoweza kuwaletelezea ufukarisho katika maisha yao ya sasa na baadae?
- Serikali inawezaje kuwasaidia wananchi wajitoe katika ajira zilizo hatari au zisizoidhinishwa kisheria na kujiunga na aina zingine za kujikimu?

5. Mabadiliko ya Kiuchumi na hali inayoweza kusababisha kufukarishwa

5.1 Upatikanaji wa huduma bora za jamii na hali inayoweza kusababisha kufukarishwa

- Kuna uhusiano gani kati ya upatikanaji wa huduma bora za jamii na hali inayoweza kusababisha (mtu, kaya au jamii) kufukarishwa?
- Kutojua kusoma na kuandika kunaweza kumsababishia mtu, kaya au jamii kuwa na hali inayoweza kuleta ufukarisho.
- Ni kwa jinsi gani uzorotaji katika huduma ya jamii kumezidisha hali inayoweza kuleta ufukarisho?

5.2 Mabadiliko ya sera.

- Kuondolewa ghafla kwa mikopo ya pembejeo za kilimo kumeathiri kwa jinsi gani maendeleo ya watu au uwezekano wa jamii kuwa katika hatari ya kufukarishwa?

5.3 Mabadiliko ya Bei za Mazao ya Biashara

- Mabadiliko ya mara kwa mara ya bei za mazao ya biashara yana madhara gani kwa hali ya kimaendeleo ya wakulima wadogo wadogo?

6. Uongozi bora na hali inayoweza kusababisha kutetereka kimaisha

6.1 Rushwa:

- Ni kwa jinsi gani rushwa huathiri huduma za jamii na kuwaweka watu katika hatari ya kufukarishwa?
- Ni kwa jinsi gani rushwa huathuri uwezekano wa vikundi mbalimbali vya kijamii katika kupata huduma za jamii?
- Watu wanatoa ushauri gani juu ya kukomeshwa kwa rushwa katika utoaji wa huduma za jamii?

6.2 Sera zisisoleta uwiano kati ya Wafanya biashara wakubwa ukilinganisha na wadogo (mfano: wavuvi, wachimba madini wadogowadogo).

- Kuna makundi ya jamii yanayo jihisi kutengwa na mielekeo ya sera kwa ujumla pamoja na sera za kupunguza umaskini?
- Jamii inaona kama serikali katilka ngazi mbalimbali imetekwa kimawazo na makundi ya matajiri wachache?
- Kutokusikika kwa sauti za makundi fulanifulani ya jamii katika kutengeneza sera, kuna athiri vipi kushuka au kutetereka kimaisha?
-

7. Uwezo/Sauti katika jamii na hali ya kufukarishwa

- Ni jinsi gani kutokuhusishwa kwa baadhi ya kaya au makundi ya jamii katika kufanya maamuzi (uwezo, kutokusikilizwa) yanavyohusiana na kuathirika kwao na hatimaye maisha yao kubadilika au kuwa katika hatari ya kufukarishwa.
- Ni aina gani za kutohusishwa kwa baadhi ya makundi ya kijamii ambazo zinaongeza kuathirika kwa makundi ya kijamii
- Ni makundi yapi yanayoguswa au kuumizwa zaidi na kutengwa au kutokuwa na sauti katika kaya au jamii katika kufanya maamuzi?

8. Unyanyasaji unaoleta madhara ya kimwili na uwezekano wa kufukarishwa

- Ni aina zipi za unyanyasaji unaoleta madhara ya kimwili unaofanywa dhidi ya baadhi ya makundi katika jamii? Yanayafanywa kwa makundi gani hasa (km: watoto, vijana, wanawake wazee)? Ni nini madhara yake kwa watu binafsi, kaya au jamii kwa ujumla?
- Ni kweli kuwa unyanyasaji unaoleta madhara ya kimwili ni tishio tosha kupunguza njia za mtu binafsi, kaya au jamii kuweza kujikimu na hivyo kudhoofisha amani, afya na ustawi wao?
- Ni njia zipi zinazotumika kwa mtu mmoja mmoja, kaya na jamii kwa ujumla kujilinda dhidi ya unyanyasaji unaoleta madhara ya kimwili?

9. Afya na hali ya kufukarishwa

- Kuna uhusiano gani kati ya afya na hatari ya kuingia katika ufukara?

9.1 Ukimwi

- Ni kwa vipi ukimwi unaathiri maisha ya watu, kaya na jamii?
- Je, athari za ukimwi kwa waathirika na wale wanaouguza zinatofautiana kufuatana na makundi ya watu?
- Wazazi wenye ukimwi wanawaathiri vipi watoto wao? Watoto wenye UKIMWI wanawaathiri vipi wazazi wao?
- Nini kinachoathiri ubora wa huduma zinazotolewa kwa wagonjwa wa ukimwi waliopo majumbani?
- Ni jinsi gani kaya zenye watu wenye ukimwi zinajikimu kutokana na kupoteza nguvu kazi au watu muhimu katika kaya kama wazalishaji?
- Hivi, umuhimu wa nguvu kazi zinazopotea, hutofautiana na aina ya shughuli ya uzalishaji?
- Watu wenye virusi vya ukimwi katika kaya wanaathirika vipi kutokana na kukosa huduma za jamii?
- Ni msaada gani serkali itoe kwa watu walioathirika kwa UKIMWI vijijini.

10. Mambo mengine yanayopelekea kuongeza hatari ya kuingia katika ufukara.

III: Jinsi ya Kujihami

11. Mikakati ya kujizuia au kukwepa majanga/dharura (km kuondoka katika maeneo yanayokumbwa na ukame mara kwa mara).

- Mikakati gani ya kujihami na majanga hutumiwa na mtu binafsi, kaya au jamii?
- Mikakati hii hutofautiana vipi kati ya kundi moja la jamii na lingine?
- Mikakati hii inabadilika? Kuna mikakati maalum ambayo inaonekana kuchukuliwa zaidi ya mingine? Kwa vipi? Kwa nini?
- Mbinu za kujikimu (nje ya sekta ya kilimo) zinanafasi gani katika hii mikakati?

- Ni kwa jinsi gani mahusiano kati ya wana-kaya au jamii yanaathiri au kuchangia mikakati hii ya kujihami?

12. Mikakati ya kujiandaa dhidi ya majanga na kuzuia madhara yake (mfano: kuhifadhi chakula)

- Ni hatua gani zimekuwa zikichukuliwa na watu binafsi, kaya au jamii kujiandaa dhidi ya majanga haya? Matokeo yake yamekuwaje?
- Mikakati hii (mfano: mbinu za kijamii za kukabiliana na madhara/majanga) inabadilika? Kwa jinsi gani? Kwa nini?

13. Mikakati ya kupunguza makali ya majanga (mfano: utoaji wa chakula kama kipato cha kazi fulani)

- Ni mikakati gani ambayo watu binafsi, kaya au jamii wanafanya kupunguza makali ya majanga ya ghafla au hali inayoendelea taratibu? Mikakati hiyo imekuwa na matokeo gani?
- Mikakati hiyo (kwa mfano: mbinu za kijamii za kukabiliana na majanga; za kupunguza makali ya majanga) inabadilika? Kwa vipi? Kwa nini?
- Serikali inaweza kufanya nini kuhamasisha na kusaidia hatua na maamuzi ya wanajamii wenyewe katika kukabiliana na majanga
- Mikakati gani mbadala inaweza kuchukuliwa na serikali ili kuiongezea jamii nguvu katika kukabiliana na majanga
- Hali ya kuwa na mbinu mbalimbali za kujipatia riziki (kama vile kuwa na shughuli za mjini wakati huohuo kuwa na shughuli kijijini n.k.) zina nafasi gani katika kuwezesha jamii kukabiliana na majanga?